30. Utoaji na mzunguko wa fedha za kielektroniki.
31. Kosa chini ya Sehemu hii.

## SEHEMU YA SABA

## AKAUNTI YA UDHAMINI NA AKAUNTI MAALUM

32. Akaunti ya udhamini.
33. Akaunti maalum.
34. Uendeshaji wa akaunti maalum.
35. Usimamizi wa akaunti maalum.

## SEHEMU YA NANE

## UKOMO WA MALIPO NA MIPANGO YA UHALISI WA MALIPO

36. Uhalali na nguvu ya kisheria kwa ajili ya utimilifu wa malipo.
37. Uhalali na nguvu ya kisheria ya utaratibu wa uhalisi wa malipo.

## SEHEMU YA TISA

KUFUNGA NA KUSIMAMIA UFILISI WA MASHIRIKA  
YANA YOTUMIA MFUMO WA MALIPO

38. Amri ya kufunga shirika.
39. Mfilisi na msimamizi wa kisheria kubanwa na maelekezo ya mifumo ya malipo.
40. Kipaumbele cha maelekezo ya malipo wakati wa kufunga kampuni.

## SEHEMU YA KUMI

## DHAMANA NA KUSHINDWA KUFANYA UTIMILIFU WA MALIPO

41. Utaratibu wa dhamana.
42. Utaratibu wa kufuata endapo itashindikana kuhitimishwa kwa malipo

SEHEMU YA KUMI NA MOJA  
MASHARTI YA JUMLA

43. Kuwasilisha marejesho.
44. Upatikanaji wa taarifa.
45. Usiri wa taarifa za mtoa hudurna ya mfumo wa malipo.
46. Utunzaji wa kumbukumbu za mfumo wa malipo.
47. Uhifadhi wa taarifa za mteja.
48. Muda wa kuingiza fedha kwenye akaunti ya mteja.
49. Uchunguzi, ukaguzi na usirnarnizi.
50. Kufifilisha rnakosa.
51. Kurnlinda rnlaji katika rnfumo wa rnalipo.
52. Upatikanaji wa hudurna ya mfumo wa rnalipo.
53. Makosa ya kirntandao katika rnfurno wa rnalipo.
54. Ushirikiano baina ya wasimarnizi katika rnfumo wa rnalipo.
55. Kinga.
56. Kanuni, rnaelekezo na rniongozo.
57. Masharti ya rnpito.

SEHEMU YA KUMI NA MBILI  
MAREKEBISHO YATOKANA YO  
MAREKEBISHO YA SHERIA YAHAWALA ZA FEDHA (SURA YA 215)

58. Tafhiri .
59. Marekebisho ya kifungu cha 41.
60. Marekebisho ya kifungu cha 52.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NA.4 YA 2015

NAKUBALI,

JAKAYA MRJSHO KIKWETE

*Rais*

25 Aprili, 2015

Sheria ya kuweka masharti kwa ajili ya udhibiti na usimamizi wa mifumo ya malipo, udhibiti wa nyenzo za kielektroniki, uhaulishaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki, watoa huduma ya mifumo ya malipo, uhalali wa nguvu ya sheria kwa utimilifu wa malipo, uhalali wa nguvu ya sheria kwa mipango ya uhalisi wa malipo, na kuweka masharti kwa ajili ya mambo yanayohusiana na Sheria hii.

[.....]

Imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA AWALI

Jina la Sheria  
na tarehe ya  
kuanza  
kutumika

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya mwaka 2015 na itanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri ataiteua na kuitangaza kupitia Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Tafsiri

3.-Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vmgmevyo-

Sura342

"benki" ina maana kama ilivyo kwenye Sheria ya Benki na Taasisi zaFedha;

"Benki" maana yake ni Benki Kuu ya Tanzania;

"fedha za kielektroniki" maana yake ni fedha kama ilivyowakilishwa na dai kwa mtoaji wa fedha za kielektroniki, ambayo huifadhiwa kielektroniki katika nyenzo au kifaa, iliyotolewa dhidi ya kupokea fedha taslimu kiasi ambacho si pungufu ya thamani ya fedha taslimu iliyotolewa, iliyokubalika kama njia ya malipo na watu au taasisi tofauti na mtoaji wa fedha za kielektroniki, na inaweza kukombolewa ikawa fedha taslimu;

"hudurna ya malipo kwa njia ya kielektroniki" maana yake ni hudurna ya malipo kwa njia ya kielektroniki inayotolewa na mtoa hudurna ya mfumo wa malipo aliyepewa leseni kwa mujibu wa Sheria hii;

- "kituo cha kubadilishana nyaraka za madai" maana yake ni mahali au utaratibu maalum ambao taasisi za fedha zimekubaliana kutumia katika kubadilishana maelekezo ya kufanya malipo au madai mengine ya kifedha baina yao;
- "kubadilisha" maana yake ni kubadilishana nyenzo za malipo zinazohusu kutuma, kufanya ulinganifu, kuthibitisha au kuhamisha fedha kabla ya kufanya malipo, ikiwa ni pamoja na maelekezo ya kufanya malipo halisi na kuweka ukomo wa kufanya malipo;
- "malipo ya mwisho" maana yake ni utimilifu wa uhaulishaji wa malipo ambao umefikia ukomo na haubadilishwi au hauwekewi masharti;
- "mfumo muhimu wa malipo" maana yake ni mfumo wa malipo wenye athari kubwa katika uchumi ambao usipodhibitiwa vya kutosha unaweza kusababisha au kupelekea misukosuko kwa washiriki katika mfumo wa malipo au uchumi kwa ujumla;
- "mfumo wa malipo" maana yake ni mfumo unaojumuisha nyenzo za malipo, taratibu za kibenki au za kuhaulisha fedha kati ya benki moja na nyingine au baina ya watoa huduma ya mfumo wa malipo ambao unahakikisha mzunguko wa fedha kwa mujibu wa idhini itolewayo chini ya Sheria hii;
- "mlaji" maana yake ni mtumiaji wa huduma za malipo ya kielektroniki zinazotolewa na mtoa huduma ya mfumo wa malipo;

- "mpango wa kufikia uhalisi wa malipo" maana yake ni makubaliano ya kimaandishi ya kubadilisha madai kadhaa kuwa dai moja halisi linalohitajika kulipwa na mtu au watu katika mfumo wa kubadilisha au kuhitimisha malipo;
- "mshiriki katika mfumo wa malipo" maana yake ni shirika linaloshiriki katika mfumo wa malipo kwa mujibu wa Sheria hii;
- "mtoa huduma ya mfumo wa malipo" maana yake ni shirika, linalojishughulisha peke yake au kwa kushirikiana na shirika lingine katika na kutoa huduma ya malipo ya kielektroniki iliyoidhinishwa kwa mujibu wa Sheria hii;
- "mtoaji wa fedha za kielektroniki" maana yake ni mtoa huduma ya mfumo wa malipo aliyepewa leseni ya kutoa fedha za kielektroniki na aliye na majukumu na anayewajibika na fedha hizo za kielektroniki;
- "nyenzo ya malipo" maana yake ni kifaa kilicho katika mfumo wa kielektroniki au wa kimaandishi inayotumika katika upitishaji au ulipaji wa fedha;
- "shirika" maana yake ni benki, taasisi ya fedha au shirika lolote la umma au binafsi;
- "taasisi ya fedha" ina maana kama ilivyo kwenye Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha;
- "taarifa" maana yake ni data, kumbukumbu, marejesho au nyaraka iliyo katika mfumo wowote ama katika maneno, katika maandishi, iliyorekodiwa kimuonekano, kisauti, kielektroniki, kisumaku, kiufundi, kumbukumbu za kompyuta au kumbukumbu nyingine iliyo katika hali,

Sura 342

---

chombo, kitu au kifaa chochote;

- "uhaulishaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki" maana yake ni uhamishaji wa fedha kwa njia ya temino au kifaa cha kielektroniki kutoka akaunti moja kwenda nyingine;
- "uhalisi wa malipo" maana yake ni utambuzi wa malipo halisi au utimilifu wa malipo halisi baina ya watu wawili au zaidi katika mfumo wa ubadilishanaji wa malipo au mfumo wa utimilifu wa malipo;
- "utimilifu" maana yake ni kitendo cha kulipa madai kikamilifu yatokanayo na uhaulishaji wa fedha au dhamana baina ya watu wawili au zaidi; na
- "wakala wa mtoa huduma ya mfumo wa malipo" maana yake ni mmiliki pekee au shirika ambalo limeingia mkataba wa uwakala na mtoa huduma ya mfumo wa malipo kuuza fedha za kielektroniki na kukomboa fedha taslimu zenye thamani sawa na fedha hizo za kielektroniki.

**SEHEMU YA PILI**  
**MAMLAKANAMAJUKUMUYABENKI**

Mamlakana  
majukumu ya  
Benki

4.-(1) Bila ya kuathiri masharti ya sheria nyingine yoyote, Benki itatekeleza na inayo mamlaka ya-

- (a) kutoa leseni ya mfumo wa malipo;
- (b) kudhibiti, kusimamia, kuchunguza na kukaguashughuli za mfumo wa malipo;
- (c) kutoa huduma ya utimilifu wa malipo kwa mfumo wa malipo;



- (d) kutoa huduma ya utimilifu wa malipo kwa kituo cha kubadilishana nyaraka za madai, na kwa kituo kikuu cha uhifadhi wa dhamana;
- (e) kumiliki na kuendesha mfumo wa utimilisho wa malipo ufanyikao kwa muda halisi;
- (f) kuratibu shughuli za mfumo wa malipo kwa kushirikiana na wadau husika;
- (g) kushiriki katika uendeshaji wa mfumo unaojumuisha nyenzo za malipo na mfumo wa utimilisho wa malipo baina ya benki na benki; na
- (h) usimamizi wa mfumo wa malipo kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, neno "hifadhi kuu ya dhamana mbalimbali" linamaanisha chombo au taasisi ya kuhifadhi dhamana, ambayo inawezesha miamala ya dhamana ihifadhiwe kwa mfumo wa kielektroni.

#### SEHEMUYA TATU MFUMO WA MALIPO

Marufuku  
kuendesha  
mfumo wa  
malipo

**5.** Mtu haruhusiwi kuendesha mfumo wa malipo bila leseni iliyotolewa na Benki kwa mujibu wa Sheria hii.

Stahiki ya  
leseni ya  
mfumo wa  
malipo

6.-(1) Mfurno wa malipo ambao wenye sifa zifuatazo unaweza kupewa leseni-

- (a) ubadilishaji wa maelekezo ya malipo baina ya taasisi za fedha ambazo ni washiriki katika mfurno;
  - (b) utimilifu wa majukumu ya malipo yanayotokana na ubadilishaji wa maelekezo ya malipo;
  - (c) uhaulishaji wa fedha kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine kwa kutumia kifaa chochote cha kielektroniki;
  - (d) uhaulishaji wa fedha za kielektroniki kutoka kwenye kifaa kimoja cha kielektroniki kwenda kwenye kifaa kingine;
  - (e) kutoa huduma za kiteknolojia ili kuwezesha uhamishaji, upelekeaji, ubadilishaji, usimamizi wa data kwa ajili ya, au kwa niaba ya mtoa huduma wa mfurno wa malipo;
  - (f) uwezesaji wa utendaji kazi wa pamoja wa mifurno ya malipo na huduma baina ya watoa huduma wa mfumo wa malipo na walaji;
  - (g) utoaji wa huduma za malipo ya kielektroniki kwa watu wasio na huduma za kibenki na walio na huduma hafifu za kibenki;
  - (h) kuanzisha kituo cha kubadilishana nyaraka za madai;
  - (i) utoaji wa mtandao wa mawasiliano ya kifedha; au
- U) malengo mengine yoyote yatakayoainishwa na Benki.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, neno "utendaji kazi wa pamoja" maana yake ni uhaulishaji wa maelekezo za malipo ama fedha bila kizuizi chochote kutoka akaunti ya mtoa huduma wa malipo mmoja ama mtumiaji kwenda kwa mtoa huduma wa malipo mwingine au mtumiaji wa akaunti ya mtoa huduma mwingine.

Maombiya  
leseni ya  
mfumo wa  
malipo

7.-(1) Asasi inayohitaji kuendesha mfumo wa malipo tapaswa kuomba leseni ya kutoa huduma ya mfumo wa malipo kwa kujaza fomu iliyoainishwa kwa madhumuni ya leseni ya mfumo wa leseni..

Maombi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1), yataambatishwa na taarifa kama zitakavyoainishwa na Benki.

(3) Benki itatoa leseni pale ambapo itaridhika kuwa muombaji ametimiza vigezo vya kupata leseni vilivyoainishwa chini ya Sheria hii pamoja na malipo ya tozo ya leseni na kukidhi masharti mengine yatakavyoainishwa na Benki.

(4) Ndani ya siku thelathini baada ya kupokea maombi ya leseni au pale ambapo taarifa za ziada zimehitajika na kupokelewa, Benki inaweza kukubali au kukataa maombi hayo.

(5) Wakati wa kutoa leseni, Benki inaweza kuweka vigezo na masharti kama itakavyoona inafaa.

(6) Leseni itadumu kwa kipindi cha miaka mitano isipokuwa kama itasitishwa au kufutwa.

(7) Endapo maombi ya leseni yamekataliwa, Benki itatoa sababu za kukataa.

(8) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (7)-

(a) muombaji, ambaye maombi yake yamekataliwa, anaweza kuomba tena endapo mapungufu yaliyofanya maombi yake yakataliwe yamerekebishwa; na

(b) Benki inaweza kukubali au kukata maombi mapya.

(9) Pale ambapo maombi yamekataliwa na muombaji hajaridhika na uamuzi kwa mujibu wa kifungu hiki anaweza kuomba kwa Gavana wa Benki mapitio ya maombi yake ndani ya siku thelathini baada ya kupokea taarifa ya kukataliwa.

Kuomba upya  
leseni ya  
mfumo wa  
malipo

**8.-** Mmiliki aliyepewa leseni chini ya Sehemu hii anaweza, ndani ya miezi sita kabla ya kumalizika muda wa leseni hiyo, kuomba upya leseni kutoka Benki.

Baada ya kupokea maombi chini ya kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kutoa upya leseni baada ya-

- (a) kupokea malipo ya ada ya leseni mpya; na
- (b) kutimiza vigezo na masharti yanayotumika katika utoaji wa leseni.

(3) Benki inaweza kukataa kutoa upya leseni endapo itaridhika kuwa muombaji alishindwa kutekeleza masharti yaliyomo kwenye leseni ya awali.

Kusimamishwa  
kwa leseni ya  
mfumo wa  
malipo

**9.-(1)** Benki inaweza kusimamisha kwa muda leseni endapo-

- (a) itajiridhisha kwamba mtoa huduma ya mfumo wa malipo ameshindwa kukidhi matakwa ya miundombinu ya mawasiliano yaliyoainishwa na Benki;
- (b) imejiridhisha kwamba shughuli za mtoa huduma ya mfumo wa malipo zinaendeshwa kwa namna ambayo inaathiri maslahi ya washiriki na watumiaji wa mifumo ya malipo; au

(c) mtoa huduma ya mfumo wa malipo amesimamishwa kwa muda kutoa huduma kwa mujibu wa sheria nyingine yoyote.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kumtaka mwenye leseni kutoa sababu kwa nini leseni yake isisimamishwe.

(3) Pale ambapo mwenye leseni ameshindwa kutoa sababu za kuridhisha, Benki inaweza kusimamisha kwa muda leseni hiyo au kutoa amri nyingine kwa namna itakavyoona inafaa.

Ufutaji wa leseni ya mfumo wa malipo

**10.-(1)** Benki inaweza kufuta leseni ya mtoaji wa huduma ya mfumo wa malipo endapo-

- (a) leseni nyingine ya mtoa huduma ya mfumo wa malipo inayohusiana na mfumo wa malipo imefutwa kwa mujibu wa sheria nyingine yoyote;
- (b) mtoa huduma ya mfumo wa malipo ameomba kwa hiari leseni yake ifutwe;
- (c) mtaa huduma ya mfumo wa malipo taarifa za kupotosha wakati wa kuomba leseni;
- (d) ameshindwa kukidhi masharti na vigezo vya leseni;
- (e) amejihusisha na rnieendo isiyo salama au isiyo ridhisha ambayo inaathiri hali yake ya kifedha au ina madhara kwa maslahi ya watoa huduma wa mfumo ya malipo au watumiaji wa huduma hizo;
- (f) amekataa kuruhusu kukaguliwa au kutoa taarifa zinazohitajika na Benki;

- (g) ameacha kufanya biashara ya mfumo ya malipo katika Jamhuri ya Muungano;
- (h) amefilisika kama ilivyoainishwa na Benki au Mahakama; au
- (i) ameshindwa kutimiza matakwa mengine yaliyomo kwenye Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kurutaka mwenye leseni kutoa sababu kwa nini leseni yake isifutwe.

(3) Pale ambapo mwenye leseni ameshindwa kutoa sababu zakuridhisha, Benki inaweza kufuta leseni hiyo au kutoa mri nyingine kwa namna itakavyoona inafaa.

Kutoa taarifa  
ya ufutwaji wa  
leseni

**11.** Endapo leseni irnefutwa kwa mjiibu wa msharti yaliyomo katika Sehemu hii, Benki-

- (a) ndani ya siku tatu za kazi baada ya tarehe ya kufutwa kwa leseni itatoa tangazo la kufutwa kupitia kwenye magazeti yenye mzunguko mkubwa katika Jamhuri ya Muungano; na
- (b) itachukua hatua nyingine stahiki kutoa taarifa kwa mjiibu kwa ujumla kuhusu kufutwa kwa leseni hiyo.

Mienendo  
isiyofaa

**12.-(1)** Mtoa huduma ya mfumo wa malipo au mshiriki wa mfumo wa malipo haruhusiwi kushiriki katika kitendo chochote ambacho kinaweza-

- (a) kusababisha athari za mifumo; au
- (b) kuathiri uadilifu, ufanisi au usalama wa mfumo wa malipo.

(2) Benki itamuelekeza mtoa huduma ya mfumo wa malipo au mshiriki wa mfumo wa malipo ambaye ameshiriki katika

kitendo kilichokatazwa na kifungu kidogo cha **(1)**, kurekebisha hali hiyo kwa namna ambayo Benki itaona inafaa.

Kusitishwa  
uongozi

- 13.-(1) Mtu ambaye yupo katika menejimenti ya mfumo wa malipo, ataondolewa kwenye nafasi hiyo endapo mtu huyo-
- (a) atakuwa ni mufilisi;
  - (b) hatiani kwa kosa linalohusiana na udanganyifu au kukosa uaminifu;
  - (c) ataondolewa kwenye cheo chake na mamlaka husika;
  - (d) atakosa akili timamu; au
  - (e) amefariki dunia.
- (2) Mtu aliyekuwa kwenye menejimenti ya mfumo wa malipo ambaye leseni yake ilifutwa, hataruhusiwa kuwa katika menejimenti nyingine ya asasi yenye kutoa huduma ya mfumo wa malipo bila idhini ya Benki.

Kosa chini ya  
Sehemu hii

- 14.** Mtu yeyote atakayekiuka masharti yoyote katika Sehemu hii, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia na endapo kosa limetendwa na -
- (a) mtu binafsi, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja; au
  - (b) asasi, itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano.

SEHEMU YA NNE  
NYENZO ZA MALJPO

Marufuku ya  
kutoa nyenzo  
za malipo bila  
idhini

- 15.-(1)** Mtu hatatoa nyenzo ya malipo ya kielektroniki bila kuwa na leseni au idhini iliyotolewa na Benki.

---

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Benki itatoa leseni kwa muombaji wa kutoa huduma ya mfumo wa malipo ambaye si taasisi ya kifedha na itatoa idhini kwa mwombaji wa kutoa huduma ya mfumo wa malipo ambaye ni taasisi ya kifedha.

Sifa stahiki za  
nyenzo ya  
malipo

**16.** Nyenzo ya kielektroniki ya malipo ambayo ina moja kati ya sifa zifuatazo inaweza kupewa leseni au kuidhinishwa na Benki endapo inaweza-

- (a) kuagiza au kuhaulisha maelekezo ya malipo;
- (b) kutunza taarifa kwenye kifaa kwa ajili ya kutuma malipo;
- (c) kutumiwa na kukubalika kwa ajili ya kuhitimisha malipo kwenye kituo cha mauzo, vituo vya wauzaji au kwenye mdahalishi; au
- (d) kuwa na sifa nyingine zozote kama ambavyo Benki itakavyoainisha.

Maombi ya  
leseni au idhini  
ya kutoa  
nyenzo ya  
malipo

**17.-(1)** Mtoa huduma ya mfumo wa malipo anayetaka kutoa nyenzo ya malipo anapaswa kuomba leseni au idhini kupitia fomu iliyoainishwa na Benki.

(2) Maombi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha **(1)**, yataambatishwa na taarifa kama itakavyoainishwa na Benki.

(3) Benki itatoa leseni au idhini endapo itaridhika kuwa muombaji ametimiza vigezo vya upatikanaji wa leseni au idhini na amekidhi matakwa mengine yatakayoainishwa na Benki.

(4) Ndani ya siku kumi baada ya kupokea maombi au endapo taarifa za ziada zilizohitajika na kupokelewa, Benki inaweza kukubali au kukataa maombi hayo.

(5) Endapo maombi yatakataliwa, Benki sababisha sababu zakukataa.



(6) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (5)-

(a) muombaji, ambaye maombi yake yamekataliwa, anaweza kuomba tena endapo mapungufu yaliyofanya maombi yake yakataliwe yamerekebishwa; na

(b) Benki inaweza kukubali au kukata maombi rnapya.

(7) Pale ambapo maombi yamekataliwa na muombaji hajaridhika na uamuzi huo anaweza kuomba Gavana wa Benki kufanya mapitio ya maombi yake ndani ya siku thelathini baada ya kupokea taarifa ya kukataliwa.

Kusimamishwa  
kwa leseni au  
idhini ya kutoa  
nyenzo ya  
malipo

**18.-(1)** Benki inaweza kusimamisha leseni au idhini ya kutoa nyenzo ya malipo endapo itajiridhisha kwamba -

(a) mtoa huduma ya mfumo wa malipo ameshindwa kukidhi matakwa ya kutoa nyenzo ya malipo;

(b) nyenzo ya malipo inaathari kwa maslahi ya watumiaji wa mifumo ya malipo; au

(c) mtoa huduma ya mfumo wa malipo alisimamishwa kwa muda kutoa huduma kwa mujibu wa sheria nyingine yoyote.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kumtaka mwenye leseni kutoa sababu kwa nini leseni yake isisimamishwe.

(3) Pale ambapo mwenye leseni ameshindwa kutoa sababu zakuridhisha, Benki inaweza kusimamisha kwa muda leseni hiyo au kutoa amri nyingine kwa namna itakavyoona inafaa.

---

Ufutaji wa  
leseni au idhini  
ya kutoa  
nyenzo ya  
malipo

**19.-(1)** Benki inaweza kufuta leseni au idhini ya kutoa nyenzo ya malipo endapo-

- (a) leseni au idhini nyingine ya kutoa huduma ya mifumo wa malipo inayohusiana na mifumo ya malipo irnefutwa kwa mrejibu wa sheria nyingine yoyote;
- (b) kutoa huduma ya mifumo wa malipo ameomba kwa hiari leseni au idhini ya kutoa nyenzo ya malipo yake ifutwe;
- (c) kutoa huduma ambetoa taarifa za uongo au za kupotosha wakati wa kuomba leseni au idhini; au
- (d) kutoa huduma ambeshindwa kukidhi msharti na vigezo vya leseni au idhini.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kutoa noti ya siku saba kurutaka mwenye leseni kutoa sababu kwa nini leseni yake isifutwe.

(3) Pale ambapo mwenye leseni ambeshindwa kutoa sababu zakuridhisha, Benki inaweza kufuta leseni hiyo au kutoa ambiri nyingine kwa namna itakavyoona inafaa.

Kosa chini ya  
Sehemu hii

**20.** Mtu yeyote aliyekiuka msharti yoyote chini ya Sehemu hii, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia binafsi na endapo kosa linaendwa na -

- (a) mtu, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja; au
- (b) asasi, litawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano.

SEHEMUYA TANO  
HUNDI ZA KIELEKTRONIKI

Uwasilishaji  
wahundi

21. Mtu yeyote anaweza kuwasilisha hundi kwa njia ya kielektroniki katika mfumo wa malipo.

Uwasilishaji  
wa hundi kwa  
njia ya  
kielektroniki

22.-(1) Benki itaainisha namna ya kuwasilisha hundi kwa njia ya kielektroniki kupitia kituo cha kubadilishana nyaraka za madai.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), benki inaweza kuwasilisha hundi kwa ajili ya malipo kwenye benki husika, kwa kuwasilisha viashiria muhimu vya hundi husika kwa njia ya kielektroniki badala ya kuwasilisha hundi yenyewe.

Kukubalika  
mahakamani  
kwa viashiria  
vya  
kielektroniki  
vya hundi

23. Katika shauri mahakamani, baraza au shauri lolote lenye asili ya kimahakama, hundi au nakala ya hundi iliyothibitishwa au viashiria muhimu vya hundi vilivyotolewa kielektroniki kuhusiana na shauri lililopo mahakamani, baraza au shauri la kimahakama vitakubalika kama ushahidi.

SEHEMU YA SITA  
FEDHA ZA KIELEKTRONIKI

Marufuku  
kutoa fedha za  
kielektroniki  
bila leseni au  
idhini

24.-(1) Mtu hataruhusiwa kutoa fedha za kielektroniki hila ya kuwa na leseni au idhini ya utoaji wa fedha za kielektroniki iliyotolewa na Benki.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Benki itatoa kwa muombaji wa huduma ya mfumo wa malipo kwa muombaji ambaye-

- (a) si benki au si taasisi ya kifedha, leseni; na
- (b) ni benki idhini.

Sifa stahiki za kutoa fedha za kielektroniki

**25.** Benki itaainisha sifa stahiki kwa mtoaji wa fedha za kielektroniki ambazo zitajumuisha muundo wa asasi, huduma zinazoruhusiwa kutolewa na kiwango cha mtaji.

Maombiya leseni au idhini ya utoaji wa fedha za kielektroniki

26.-(1) Mtu ambaye anakusudia kutoa fedha za kielektroniki atapaswa kuomba leseni au idhini ya utoaji wa fedha za kielektroniki kupitia fomu itakayoainishwa na Benki.

(2) Maombi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) yataambatishwa na taarifa kama itakavyoainishwa na Benki.

(3) Benki itatoa leseni au idhini pale ambapo itaridhika kuwa muombaji ametimiza vigezo vya upatikanaji wa leseni au idhini kama vilivyoainishwa chini Sheria hii na kukidhi masharti mengine yatakayoainishwa na Benki.

(4) Ndani ya siku thelathini baada ya kupokea maombi ya leseni au idhini au pale ambapo taarifa za ziada zilizohitajika zimepokelewa, Benki inaweza kukubali au kukataa maombi hayo.

(5) Benki inaweza, pale ambapo inatoa leseni au idhini, kuweka vigezo na masharti kama itakavyoona inafaa.

(6) Leseni au idhini itadumu kwa kipindi cha miaka mitano isipokuwa kama itasimamishwa au kufutwa.

(7) Endapo maombi yatakataliwa, Benki itatoa sababu za kuyakataa.

(8) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (7)-

(a) muombaji, ambaye maombi yake yamekataliwa anaweza kuomba tena endapo upungufu uliosababisha maombi yake yakataliwe yamerekebishwa.

(b) Benki inaweza kukubali au kukata maombi mapya.

(9) Pale ambapo maombi yamekataliwa na muombaji hajaridhika na uamuzi huo anaweza kuomba kwa Gavana wa Benki kufanya mapitio ya maombi yake ndani ya siku thelathini baada ya kupokea taarifa ya kukataliwa.

Kuomba upya leseni au idhini ya utoaji wa fedha za kielektroniki

**27.-** Mmiliki wa leseni au idhini ya utoaji wa fedha za kielektroniki chini ya Sehemu hii anaweza kuomba upya leseni kutoka Benki miezi sita kabla ya kumalizika muda wa leseni au idhini hiyo.

Baada ya kupokea maombi chini ya kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kutoa upya leseni au idhini baada ya-

(a) kupokea malipo ya ada ya leseni mpya; na

(b) kutimiza vigezo na masharti yanayotumika katika utoaji wa leseni.

(3) Benki inaweza kukataa kutoa leseni au idhini mpya endapo muombaji ameshindwa kutekeleza masharti yaliyomo kwenye leseni au idhini ya awali.

Kusimami sha kwa muda leseni au idhini ya kutoa fedha za kielektroniki

**28.-(1)** Benki inaweza kusimamisha kwa muda leseni au idhini ya kutoa fedha za kielektroniki endapo-

(a) imejiridhisha kwamba shughuli za mtoaji wa fedha za kielektroniki zinaendeshwa kwa namna ambayo inaathiri usalama wa mfumo wa fedha au watumiaji fedha za kielektroniki; au

(b) mtoa huduma ya mfumo wa malipo amesimamishwa kwa muda kutoa huduma kwa mujibu wa sheria nyingine yoyote.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kumtaka mwenye leseni au idhini kutoa sababu kwa nini leseni au idhini yake isisimamishwe.

(3) Pale ambapo mwenye leseni au idhini ameshindwa kutoa sababu zakuridhisha, Benki inaweza kusimamisha kwa muda leseni au idhini hiyo au kutoa amri nyingine kwa namna itakavyoona inafaa.

Kufutwa kwa leseni au idhini ya kutoa fedha za kielektroniki

**29.-(1)** Benki inaweza kufuta leseni au idhini ya mtoaji wa fedha za kielektroniki endapo kuhusiana na mtoaji wa fedha za kielektroniki-

- (a) leseni au idhini yake nyingine inayohusiana na mfumo wa malipo imefutwa kwa mujibu wa sheria nyingine yoyote;
- (b) yeye mwenyewe ameomba kwa hiari leseni au idhini yake ifutwe;
- (c) ametoa taarifa za uongo au za kupotosha wa kuomba leseni au idhini;
- (d) ameshindwa kukidhi masharti na vigezo vya leseni au idhini au ameshindwa kukidhi masharti ya maboresho yaliyotakiwa chini ya Sheria hii;
- (e) amejihusisha na mienendo Islyo salama au isiyoridhisha ambayo inaathiri hali yake ya kifedha au ina madhara kwa maslahi ya watoa huduma wa mifumo ya malipo au watumiaji wa huduma hizo;
- (f) amekataa kuruhusu kukaguliwa au kutoa taarifa zinazohitajika na Benki ama vinginevyo amekiuka masharti ya Sheria hii;

- (g) ameacha kufanya biashara ya mifumo ya malipo katika Jamhuri ya Muungano;
- (h) amefilisika kama ilivyoamuliwa na Benki au mahakama; au
- (i) ameshindwa kutimiza matakwa mengine yaliyomo kwenye Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha **(1)**, Benki inaweza kutoa notisi ya siku saba kumtaka mwenye leseni au idhini kutoa sababu kwa nini leseni au idhini yake isifutwe.

(3) Pale ambapo mwenye leseni au idhini ameshindwa kutoa sababu zakuridhi sha, Benki inaweza kufuta leseni au idhini hiyo au kutoa anri nyingine kwa namna itakavyoona inafaa.

Utoaji na  
mzunguko wa  
fedha za  
kielektroniki

**30.-(1)** Mtoaji wa fedha za kielektroniki aliyepewa leseni au idhini ya kutoa fedha za kielektroniki atapaswa kuzingatia yafuatayo -

- (a) atatoa fedha za kielektroniki baada tu ya fedha taslimu zenye thamani sawa na fedha za kielektroniki kuwekwa katika akaunti ya udhamini au akaunti maalumu kwa mujibu wa Sheria hii;
- (b) atahakikisha kwamba fedha za kielektroniki zilizotolewa zinalingana na fedha taslimu zilizopo kwenye akaunti ya udhamini au akaunti maalumu kwa mujibu wa Sheria hii;
- (c) atawasilisha Benki kwa njia ya kielektroniki, majina ya wote walioandiki shwa na watumiaji wa fedha za kielektroniki ambao fedha zao zipo kwenye akaunti ya udhamini, katika muda utakaoainishwa; na
- (d) atatimiza masharti, kama ambavyo Benki itaainisha kwa kanuni.

(2) Kukombolewa kwa fedha taslimu kutoka kwenye fedha za kielektroniki au kununua fedha za kielektroniki kunaweza kufanyika kwa wakala chini ya mkataba wa uwakala baina ya mtoa huduma ya mfumo wa malipo aliye na leseni au idhini ya kutoa fedha za kielektroniki.

(3) Benki itaainisha kanuni za uwakala za kusimamia utendaji wa wakala, ambazo zitajumuisha masharti yanayokidhi masharti ya sheria ya kuzuia fedha haramu, mahitaji ya ukwasi namna ya kumtambua aina ya mteja, huduma kwa mteja.

Kosa chini ya Sehemu hii

**31.** Mtu yeyote atakayekiuka sharti lolote chini ya Sehemu hii, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia na endapo kosa limetendwa na-

- (a) mtu binafsi, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini au kifungo kisichopungua miaka rnitano au vyote kwa pamoja; au
- (b) asasi, itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano.

#### SEHEMU YA SABA

#### AKAUNTI YA UDHAMINI NA AKAUNTI MAALUM

Akaunti ya Udhadini

**32.** Mtoa huduma ya mfumo wa malipo mwenye leseni ambaye si asasi ya kibenki au si asasi taasisi ya kifedha yenye leseni ya kutoa fedha za kielektroniki itapaswa kufungua na kuendesha akaunti ya udhamini kwa mujibu wa Sheria hii.

Akaunti Maalum

**33.** Mtoa huduma ya mfumo wa malipo mwenye leseni ambaye ni benki au asasi ya kibenki yenye leseni ya kutoa fedha za kielektroniki itapaswa kufungua na kuendesha akaunti maalum kwa mujibu wa Sheria hii.



Uendeshaji  
wa akaunti  
maalum

**34.-(1)** Mtoaji wa fedha za kielektroniki mwenye leseni aliyerejewa katika kifungu cha 32 atapaswa kuanzisha asasi nyingine ya kisheria na yenye muundo wa asasi ya udhamini kwa ajili ya kuendesha akaunti ya udhamini, na ambayo muundo wake na uendeshaji wake kiutawala utaidhinishwa na Benki-

(2) Asasi yenye mamlaka kisheria iliyoainishwa kwenye kifungu kidogo cha (1)-

- (a) itawasilisha Benki maombi ya kufungua akaunti ya udhamini kwa kutumia fomu iliyoainishwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa fedha za kielektroniki katika benki;
- (b) itaingia mkataba wa akaunti ya udhamini na benki kama itakavyobainishwa katika kanuni; na
- (c) itafungua akaunti ya udhamini katika benki kwa ajili ya kutunza fedha za wateja walionunua fedha za kielektroniki kutoka kwa mtoaji wa fedha za kielektroniki;

(3) Mtoa fedha za kielektroniki na asasi yenye mamlaka ya kisheria iliyorejewa katika kifungu kidogo cha (1)-

- (a) hazitachanganya au kutumia fedha zilizomo kwenye akaunti ya udhamini na fedha za shughuli nyingine;
- (b) zitaweka utaratibu wa usalama wa kulinda fedha zilizomo kwenye akaunti ya udhamini dhidi ya madhara yanayoweza kusababisha hasara kwa fedha za wanufaika;
- (c) zitadhibiti madhara ya kutunza akaunti ya udhamini kwa kufungua akaunti hiyo katika benki mbalimbali kama itakavyoainishwa na Benki;
- (d) zitahakikisha kwamba riba yoyote inayopatikana kwenye akaunti ya udhamini inarinnufaisha moja kwa moja mteja kama itakavyoainishwa na Benki;

- (e) zitakagua na kuchapisha taarifa za fedha zinazohusiana na asasi ya udhamini kuhusiana na akaunti ya udhamini;
  - (f) zitahakikisha kwamba maelekezo ya kutoa fedha kwenye akaunti ya udhamini yanazingatiwa;
  - (g) zitahakikisha kwamba wakati wote fedha zilizopo katika akaunti ya udhamini zinalingana na fedha za kielektroniki zilizotolewa; na
  - (h) zitazingatia matakwa mengine yoyote ambayo Benki itaainisha.
- (4) Mtu yeyote atakayekiuka sharti lolote chini ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia na endapo kosa limetendwa na-
- (a) mtu binafsi, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja; au
  - (b) asasi, itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano.

Usimamizi  
wa akaunti  
maalum

**35.-(1)** Mtoa fedha za kielektroniki mwenye leseni aliyerejewa katika kifungu cha 33-

- (a) atawasilisha Benki taarifa ya kufungua akaunti maalum iliyo katika fomu iliyoainishwa ya kufungua akaunti maalum, kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa fedha za kielektroniki;
- (b) atafungua akaunti maalum kwa ajili ya kutunza amana za wateja walionunua fedha za kielektroniki kutoka kwa mtoaji wa fedha za kielektroniki;
- (c) atahakikisha kwamba akaunti hii ina taarifa za wateja wote wanaopata huduma ya fedha za kielektroniki;

- (d) atahakikisha kwamba akaunti maalum inalindwa dhidi ya athari ambayo inaweza kusababisha hasara kwa wanufaika wa fedha; na
  - (e) atatimiza matakwa mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Benki.
- (2) Mtu yeyote atakayekiuka sharti lolote chini ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia na endapo kosa limetendwa na-
- (a) mtu binafsi, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini au kifungo kisichopungua miaka mitano au vyote kwa pamoja; au
  - (b) asasi, itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano.

#### SEHEMU YA NANE

##### UKOMO WA MALIPO NA MIPANGO YA UHALISI WA MALIPO

Uhalali,  
nguvu ya  
kisheria na  
utimilifu wa  
malipo

36.-(1) Agizo la kufanya malipo au utimilifu wa uhaulishaji wa malipo katika mfumo wa malipo utakuwa halali na utakuwa na nguvu ya kisheria.

(2) Agizo la kufanya malipo au utimilifu wa malipo kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) utatimilika, hautabatilika na hautafutwa na mtu yeyote kuanzia pale agizo la kufanya malipo au utimilifu wa malipo ulipothibitishwa kuwa timilifu katika mfumo wa malipo.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2), Benki itaainisha namna ya kushughulikia maagizo ya malipo au utimilifu wa malipo yaliyofanywa kimakosa.

(4) Endapo Benki itaona kwamba kuna uwezekano wa kutokea athari ya kimfumo wakati wa kufanya malipo au utimilifu

wa malipo uliorejewa katika kifungu kidogo cha (1), Benki-

(a) itazuia ufanyaji au uhamishaji wa maelekezo ya malipo au itatengua malipo au uhaulishaji;

(b) itatoa taarifa ya maandishi kwa washiriki wa mfumo wa malipo ikielezea sababu ya kuzuia au kutengua malipo hayo au uhaulishaji wa malipo.

(5) Muamala wowote uliofanyika kwa kukiuka masharti ya kifungu hiki utakuwa ni batili.

Uhalali na nguvu ya kisheria ya utaratibu wa uhalisi wa malipo

**37.-(1)** Utaratibu wa uhalisi wa malipo katika mfumo wa malipo utakuwa halali na utakuwa na nguvu ya kisheria.

(2) Jukumu lolote la utimilifu halisi wa malipo la mtoa huduma au mshiriki katika mfumo wa malipo katika utaratibu wa uhalisi wa malipo ambao haujatimilika utakuwa ni madai yanayoweza kuthibitishwa katika shauri la ufilisi na kulipwa kwa wanufaika.

#### SEHEMU YA TISA

#### KUFUNGA NA KUSIMAMIA UFILISI WA MASHIRIKA YANA YOTUMIA MFUMO WA MALIPO

Amriya kufunga shirika Sura ya 212 Suraya 342

**38.-(1)** Amri ya kufunga shirika, au kuliweka chini ya usimamizi wa mahakama au wa kisheria, kulingana na masharti ya Sheria ya Makampuni au Sheria nyingine yoyote ya ufilisi iliyotolewa kwa mshiriki wa mfumo wa malipo, itawasilishwa Benki mapema iwezekanavyo.

(2) Amri inayorejewa katika kifungu kidogo cha (1), haitaathiri utimilifu wowote wa malipo au maagizo ya malipo

katika mfumo wa malipo yaliyofanywa kabla ya kutolewa kwa amri hiyo.

Mfilisi na  
msimamizi  
wa kisheria  
kubanwa na  
maelekezo ya  
mifumo ya  
malipo  
Sura ya 212  
Sura ya 342

39.-(1) Bila kujali jambo lolote lililo kinyume katika Sheria ya Makampuni au sheria nyingine yoyote ya ufilisi, pale ambapo amri imetolewa ya kufunga au kumweka mshiriki wa mfumo wa malipo chini ya usimamizi wa mahakama au wa kisheria, wajibu wowote au utimilifu wa malipo yanayoelekezwa kwa mshiriki wa mfumo wa malipo ambayo-

- (a) yaliamuliwa kabla ya kutolewa kwa amri;
- (b) yalitakiwa kutimilika, kuhaulishwa, wakati au baada ya kutoka kwa amri; au
- (c) yalikuwa yanategemewa kutimilika katika tarehe ilipotolewa amri hiyo,

yatambana mfilisi wa mshirika wa mfumo wa malipo, msimamizi wa mahakama au msimamizi wa kisheria.

(2) Kifungu kidogo cha (1), kitatumika kwa majukumu yoyote ya malipo au utimilifu wa malipo ambayo-

- (a) yaliamuliwa kabla ya kutolewa kwa amri hiyo;
- (b) yalitakiwa kutimilika, kuhaulishwa wakati au baada ya kutolewa kwa amri hiyo; au
- (c) yalikuwa yanategemewa kwa ajili ya utimilifu katika tarehe ilipotolewa amri hiyo.

Kipaumbele  
cha  
maelekezo ya  
malipo  
wakati wa  
kufunga  
kampuni  
Sura ya 212

40.-(1) Bila kujali jambo lolote lililo kinyume cha Sheria ya Makampuni au Sheria nyingine yoyote ya ufilisi, pale ambapo-

- (a) mshiriki wa mfumo wa malipo atakuwa amefilisiwa; na

- (b) kuna maelekezo ya kufanya malipo ambayo hayajakamilika yaliyoelekezwa kwa mshiriki wa mfumo wa malipo na yalifanyiwa uhalisi katika mfumo wa malipo kabla ya kutolewa kwa amri ya kufilisi,

maelekezo hayo ya malipo ambayo hayajakamilika yatalipwa kutoka kwenye mali za mshiriki huyo wa mfumo wa malipo, na yatapewa kipaumbele cha juu dhidi ya madeni yote yale yasiyo na dhamana kutoka katika mali za mshiriki huyo.

(2) Kifungu kidogo cha (1), hakitatafsiriwa kuruhusu maelekezo ya malipo yalipwe kwa kipaumbele cha juu dhidi madeni mengine yoyote dhidi ya mali, pale ambapo maelekezo yalithibitishwa na mshiriki huyo wa mfumo wa malipo au ilikusudiwa kumpa mwenye hati ya malipo maelekezo yenye kipaumbele dhidi ya washirika wengine wa mfumo wa malipo au wadai wengine.

#### SEHEMU YA KUMI

#### DHAMANA NA KUSHINDWA KUFANYA UTIMILIFU WA MALIPO

Utaratibu wa  
dhamana

**41.-(1)** Benki itaainisha namna ya kutunza mali za kutosha katika hali ya kifedha kama dhamana kwa ajili ya kudhamini madeni au majukumu ya malipo ya mshiriki wa mfumo wa malipo kwa ajili ya kutimiza wajibu wake wa malipo.

(2) Dhamana iliyorejewa katika kifungu kidogo cha (1)-

- (a) itauzwa ili kutekeleza wajibu wa mshiriki wa mfumo wa malipo kutokana na kushindwa kutimiza wajibu wake wa kuhitimisha malipo; na
- (b) italindwa dhidi ya ufili si.

(3) Mshiriki wa mfumo wa malipo ambaye anaendesha mfumo wa malipo bila dhamana ya kutosha, akipatikana na hatia, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano.

Utaratibu wa kufuata endapo itashindikana kuhitimisha malipo

42.-(1) Mtoa huduma wa mfumo wa malipo ataweka utaratibu wa kushindwa kuhitimisha malipo wa kimaandishi utakaoainisha jinsi ambavyo kushindwa kuhitimisha malipo kutadhibitiwa endapo mmoja au baadhi ya washiriki katika mfumo wa malipo atashindwa kuhitimisha malipo.

(2) Mtoa huduma ya mfumo wa malipo atawasilisha Benki kimaandishi utaratibu wa kushindwa kuhitimisha malipo uliorejewa katika kifungu kidogo cha (1).

#### SEHEMU YA KUMI NA MOJA MASHARTI YA JUMLA

Kuwasilisha marejesho

43.-(1) Mtoa huduma ya mfumo wa malipo atawasilisha marejesho yanayohusiana na uendeshaji wa mfumo wa malipo au huduma kama itakavyoainishwa na Benki.

(2) Benki inaweza kutumia au kutoa taarifa iliyoipokea chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa ajili ya matumizi ya umma.

(3) Benki inaweza kumtoza mtu atakayekiuka masharti ya kifungu hiki faini ya shilingi milioni kumi kwa kila siku ya ukiukwaji wa sharti hili, na faini hii inaweza kutolewa kutoka kwenye bakaa iliyo Benki au kupitia utaratibu mwingine wa kisheria .

Upatikanaji wa taarifa

44.-(1) Benki itakuwa na uwezo wa kupata taarifa inayohusiana na mfumo wowote wa malipo na inaweza kuelekeza taarifa iwasilishwe na mtoa huduma ya mfumo wa malipo kwa maandishi ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya maombi .

(2) Benki inaweza kumtoza mtu atakayekiuka masharti ya kifungu hiki faini ya shilingi milioni kumi kwa kila siku ya ukiukwaji wa sharti hili, na faini hii inaweza kutolewa kutoka kwenye bakaa iliyo Benki au kupitia utaratibu mwingine wa kisheria.

Usiri wa taarifa za mtoa huduma yamfumo wa malipo

**45.-(1)** Taarifa iliyopatikana kwa mujibu wa kifungu cha 44 itakuwa ni siri na haitatolewa na mkurugenzi au afisa yeyote wa Benki isipokuwa kama taarifa hiyo inahitajika kwa mujibu wa sheria.

(2) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), Benki inaweza kutoa taarifa yoyote kwa wakala mwingine mwenye jukumu la kudhibiti au kusimamia mifumo ya malipo inayotokana na mkataba wa kupeana taarifa, ama ndani ya Jarnhuri ya Muungano au nje ya nchi, iwapo taarifa hiyo inahitajika na itatumika kwa ajili ya usimamizi au uangalizi na itaendelea kuwa siri.

Utunzaji wa kumbukumbu zamfumo wa malipo

**46.-( 1)** Mtoa huduma ya mfumo wa malipo atatunza kumbukumbu za miamala yote ya malipo kwa njia ya kielektroniki na taarifa alizozipata au alizozitengeneza wakati wa uendeshaji au usimamizi wa mfumo wa malipo kwa kipindi ambacho Benki itaainisha.

(2) Utunzaji wa kumbukumbu chini ya kifungu kidogo cha **(1)**, utakuwa kwa njia ya kielektroniki na isiyo ya kielektroniki kulingana na jinsi taarifa husika ilivyopatikana au ilivyotengenezwa ili kuzingatia utunzwaji wa taarifa katika uhalisia wake.

(3) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), mtu anayekusudia kuharibu taarifa za miamala ya malipo ya kielektroniki chini ya Sheria hii, ataomba idhini ya kuharibu taarifa hizo kutoka Benki.



(4) Mtu atakayekiuka ama kushindwa kutekeleza kifungu hiki, akipatikana na hatia, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano.

Uhifadhi wa taarifa za mteja

**47.-(1)** Bila kuathiri sheria nyingi yoyote, mtoa huduma ya mfumo wa malipo-

- (a) atalinda usiri wa taarifa za mshiriki na taarifa za mteja wa mfumo wa malipo; na
- (b) hatatoa taarifa za mshiriki au mteja wa mfumo wa malipo isipokuwa kwa mujibu wa sheria, amri ya mahakama au kwa ridhaa ya mteja husika.

(2) Mtu atakayekiuka ama kushindwa kutekeleza kifungu hiki, akipatikana na hatia, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia moja.

Muda wa kuingiza fedha kwenye akaunti ya mteja

**48.-(1)** Mtoa huduma wa malipo, mara baada ya kupokea malipo kwenye akaunti yake ya uhitimisho wa malipo, yanayomiliki mteja yake, atazingiza fedha IZO mapema Iwez anavyo wenye akaunti ya mteja.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Benki itaainisha muda muafaka wa kuingiza fedha kwenye akaunti ya mteja kulingana na aina ya mfumo wa malipo.

(3) Mtu ambaye amekiuka kifungu hiki, atalipa faini ya kiasi cha asilimia kumi na tano ya fedha alizocheleweshwa kwa kila siku.

Uchunguzi, ukaguzina usimamizi

**49.-(1)** Kwa madhumuni ya kufanya uchunguzi, ukaguzi na usimamizi chini ya Sheria hii, Benki inaweza kuidhinisha maafisa wake kwa maandishi-

- (a) kuingia na kupekua eneo la mtu ambaye Benki ina sababu ya kuamini anatoa au anaendesha mfumo wa malipo au anatoa huduma ya kielektroniki kinyume na Sheria hii;
- (b) kukagua vitabu, kompyuta, seva, akaunti na kumbukumbu au kuchukua kitu chochote muhimu au taarifa itakayosaidia katika kumchunguza mtu huyo na kuchukua nakala au kutoa dondo zake; na
- (c) kumsimamia mtoa huduma wa mfumo wa malipo pamoja na athari zinazoambatana na mfumo huo.

(2) Katika kumsimamia mtoa huduma wa mfumo wa malipo anayefanya shughuli zake ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano, Benki inaweza kuingia makubaliano na taasisi ya usimamizi kwa ajili ya kubadilishana taarifa za usimamizi ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano.

Kufifi lisha  
makosa

**50.-(1)** Gavana wa Benki au afisa mahususi aliyeruhusiwa na Gavana wa Benki kwa kupitia taarifa iliyochapisha ndani ya *Gazeti* anaweza, kulingana na matakwa ya kifungu hiki, kama emeridhika kwamba mtu ametenda kosa ndani ya Sheria hii, atajumuisha kwakupokea fedha kutoka kwa mtu huyo.

(2) Jumla ya fedha itakayolipwa katika kifungu kidogo cha (1)-

- (a) haitazidi kiwango cha juu cha faini kilichoainishwa chini ya kosa lililotendwa dhidi ya Sheria hii; na
- (b) itajumuisha gharama za Benki zitokanazo na kukamata, kutunza, kukarabati au kuondoa kitu chochote kilichochukuliwa kutokana na kosa alilotenda pamoja na malipo mengine.

(3) Mamlaka yaliotolewa katika Sheria hii yatatumiwa pale ambapo mtu atakubali kwamba ametenda kosa na amekubali

kwa maandishi kamaitakavyo ainishwa ndani ya fomu.

(4) Gavana wa Benki au afisa atakayetumia mamlaka chini ya kifungu hiki atatoa stakabadhi iliyoainishwa na fomu kwa mtu aliyetoa fedha chini ya kifungu kidogo cha (2).

(5) Fedha zozote zilizo pokelewa chini ya kifungu hiki, baada ya kutoa gharama na malipo, zitawekwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina.

(6) Pale ambapo mashauri yamefunguliwa dhidi ya mtu huyo chini ya Sheria hii, itakakua ni utetezi mzuri iwapo mtu huyo ataonyesha ushahidi kwamba kosa analotuhumiwa limefanyiwa majumuisho chini ya kifungu hiki.

(7) Amri ya kujumuisha chini ya kifungu hiki itachukuliwa kuwa ni sawa na amri ya Mahakama Kuu na kwa maana hiyo itatumika kukaza hukumu kupitia taratibu za Mahakama Kuu.

Kumlinda  
mlaji katika  
mfumo wa  
malipo

**51.-(1)** Benki itaainisha maelekezo ya kumlinda mlaji wa huduma ya mfumo wa malipo.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha **(1)**, mtoa huduma ya mfumo wa malipo atatoa-

- (a) vigezo na masharti yaliyo wazi, ya haki, vinavyosomeka, vipo katika lugha inayoeleweka na kuainisha haki na wajibu wa pande zote;
- (b) utaratibu wa kusikiliza malalamiko na utatuzi wa migogoro; na
- (c) taarifa kamili ya mambo muhimu kwa ajili ya matumizi ya huduma za malipo ya kielektroniki, ikiwa ni pamoja na bei ya bidhaa na huduma.

(3) Mtoa huduma ya mfumo wa malipo hatapaswa kutoa matangazo ya biashara yenye kupotosha mlaji au huduma ambayo hajaruhusiwa kwa mujibu wa Sheria hii.

Upatikanaji  
wa huduma  
ya mfumo wa  
malipo

52. Mtoa huduma ya mfumo wa malipo atahakikisha kwamba huduma ya mfumo wa malipo anayoitoa inapatikana kwa mtumiaji muda wote ulioidhinishwa.

Makosa ya  
kimtandao  
katika mfumo  
wamalipo

53.-(1) Mtu ambaye amepata taarifa, kumbukumbu au data za fedha za mtu mwingine, kwa kutumia kifaa cha kielektroniki, kifaa chochote, kwa mpango au mbinu ambayo imewezesha upatikanaji wa taarifa au data kinyume na sheria, ametenda kosa.

(2) Mtu yeyoye, kwa makusudi au bila idhini ya kisheria, hatatengeneza, hatauza, hatanunua kwa ajili ya matumizi, hataagiza au hatauza nje ya nchi, hatasambaza au hatajishughulisha na-

- (a) kifaa kilichotengenezwa au kubadilishwa kwa ajili ya kupata taarifa za kifedha;
- (b) kupata neno la siri la kompyuta, kiashiria cha siri cha kufungua au data yoyote ambayo itamwezesha mtu kupata taarifa zilizomo katika kompyuta; au
- (c) kuwa na programu ya kompyuta ili aitumie au itumike na mtu mwingine kwa lengo la kutenda kosa.

(3) Mtu ambaye amekiuka ama kushindwa kutekeleza kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya kiasi ambacho ni kikubwa kati ya shilingi milioni kumi au mara tatu ya thamani ya mali iliyoibiwa au kifungo cha miaka isiyopungua kurni na tano au vyote kwa pamoja.

Ushirikiano  
baina ya  
wasimamizi  
katika mfumo  
wamalipo

54. Benki itashirikiana na wasimamizi wengine wanaohusika na mifumo ya malipo pamoja na taasisi za Serikali katika maeneo ya ufuatiliaji na usimamizi wa mifumo ya malipo na kuongeza ufanisi wa Serikali katika malipo, malipo ya kodi na malipo mengine ya kifedha.

Kinga

**55.** Shtaka au shauri lolote halitafunguliwa dhidi ya afisa au mfanyakazi yeyote wa Benki kuhusiana na kitendo chochote kilichofanyika au kuacha kufanyika, kwa nia njema katika utekelezaji wa majukumu aliyopewa na Sheria hii.

Kanuni,  
maelekezo na  
miongozo

**56.-(1)** Gavana wa Benki anaweza kutunga kanuni na masharti na kuzichapisha kwenye *Gazeti*, ambazo hazikinzi na matakwa ya Sheria hii, kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii kwa ufanisi.

(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo (1), Gavana wa Benki anaweza kutunga Kanuni katika maeneo yafuatayo:

- (a) masharti ya leseni;
- (b) kushiriki kwenye mfumo wa malipo;
- (c) nyenzo za kielektroniki za malipo, fedha za kielektroniki, hundi za kielektroniki;
- (d) wakala wa mtoa huduma ya mfumo wa malipo;
- (e) ukomo na uhitimisho wa malipo;
- (f) utaratibu wa dhamana;
- (g) muda muafaka wa kuingiza fedha kwenye akunti ya mteja;
- (h) usimamizi wa akaunti ya udhamini;
- (i) muda wa kutunza kumbukumbu za miamala ya malipo; na
- G) matakwa ya ulinzi wa mlaji.

(3) Gavana wa Benki, bila ya kuchapisha kwenye *Gazeti*, anaweza kutoa maagizo, miongozo, viwango, amri na waraka wa kudhibiti mwenendo wa jinsi madhumuni ya Sheria hii yanaweza kutekelezwa.

Masharti ya  
mpito

**57.-(1)** Mtu ambaye amepata idhini ya maandishi kutoka Benki kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, ndani ya miezi sita tokea tarehe ya kuanza kutumika, atatakiwa kuomba leseni kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), mtu anayeendelea;

- (a) kuendesha mfumo wa malipo;
- (b) kutoa nyenzo ya malipo;
- (c) kutoa fedha za kielektroniki; au

(d) kutoa huduma nyingine yoyote ya mifumo ya malipo, baada ya miezi sita tokea tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini isiyopungua shilingi milioni mia moja au kwa kifungu kisichozidi miaka mitano; au vyote kwa pamoja.

**SEHEMU YA KUMI NA MBILI  
MAREKEBISHO YATOKANAYO  
MAREKEBISHO YA SHERIA YAHAWALA ZA FEDHA (SURA YA 215)**

Tafsiri  
Sura ya 215

**58.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Hawala za Fedha ambayo humu ndani inarejewa kama "Sheria mama".

Marekebi sho  
ya kifungu  
cha 41

**59.** Sheria mama inafanyiwa markebisho kwenye kifungu cha 41 kwa kuongeza kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(4) Bila kujali kifungu kidogo cha (1), hundi inaweza kuwasilishwa kwa njia ya kielektroniki kwenye mfumo wa malipo."

Marekebi sho  
yakifungu  
cha 52

**60.** Sheria mama inafanyiwa marekebisho kwenye kifungu cha 52 kwa kuingiza ufafanuzi ufuatao kwenye kifungu kidogo cha (4):

"Isipokuwa kwamba, kifungu kidogo hiki hakitatumika kwenye uwasilisaji wa njia ya kielektroniki wa hundi au hawala katika sheria nyingine yoyote".

Imepitishwa na Bunge tarehe 23 Machi, 2015.

THOMAS D. KASHILILAH  
Katibu wa Bunge